WAPULIZA VIPENGA PWANI WATUCHAFULIA KANDANDA

NI Jambo la dhahiri kwamba mchezo wa kandanda ama kwa lugha nyingine soka ama kabumbu ni mchezo ambao unapendwa na kuwa na wafuasi wengi zaidi kuliko michezo mingine yoyote hapa nchini na Serikali yetu inafanya kila juhudi kuona hali ya mchezo huu inakuwa ya kuridhisha na kufikia kiwango cha juu.

Na katika mambo muhimu yanayohitajika kufuatwa zaidi kwenye mchezo huu ni kuzingatiwa kwa sheria na kanuni zake na wanaohitajika kuzingatia sheria na kanuni hizo ni maafisa, wachezaji na waamuzi ambao wakijumuika pamoja ndipo hupatikana maendeleo ya kuridhisha.

Jambo la kutia moyo ni vile shirikisho la Soka (Kenya Football Federation) linavyojaribu liwezalo kuona na kuhakikisha nidhamu inadumishwa ndani na nje ya uwanja na vile inavyohukumu na kuadhibu vilabu maafisa na wachezaji wanaokiuka baadhi ya sheria na kanuni za mchezo.

Tumeshaona hatua nyingi zikichukuliwa kwa vilabu kama vile klabu moja ya Mombasa iliyopigwa marufuku kutocheza soka kwa mzima kutokana na kuzusha "vita" baada ya kushindwa. Tumefahamu wachezaji wote wa klabu hiyo pia wameadhibiwa kutocheza mpira kwa muda huo wa kipindi kimoja, ni wazi nidhamu ikidumishwa, ndipo maendeleo ya mchezo wowote yanapopatikana.

Adhabu pia zimeshawahi kutolewa kwa baadhi ya maafisa wa KFF wenyewe ambao wamekwenda kinyume na kanuni na katiba za shirikisho hilo. Na hatua kali nyingine zimechukuliwa kwa viongozi wa vilabu ambao wamefanya makosa ambayo yangehataraisha maendeleo ya vilabu vyao.

Lakini jambo linalotushangaza hapa Mombasa ni kuona Waamuzi ama kwa jina lingine wapiga vipenga wamekuwa wakifanya "madhambi" chungu nzima lakini hakuna hatua inayostahiki inayochukuliwa kwao. Je, wao wamepewa uwezo na Shirikisho La Kandanda Ulimwenguni (FIFA) wa kufanya watakavyo bila ya kuzingatia sheria na kanuni za uchezeshaji na halafu waepukane na adhabu yoyote?

Marefu wamekuwa wakionyesha udhoofu wa upigaji filimbi; udhoofu ambao mara nyingi unazusha fujo na ghasia na hata mashabiki kuwa tayari kuchapana kutokana na makosa ya waamuzi. Lakini baada ya waamuzi hao kuharibu mchezo wowote, huchukua pesa zao na kuacha timu zikishtakiana hali makosa yametokana na wao.

Wachezaji wanapocheza mchezo mbaya wa kutupa ovyo "madaluga" kwa nia ya kuumiza wenzao huadhibiwa kwa kupewa kadi nyekundu na kutolewa nje ya uwanja na baadaye kukosa mechi mbili zitakazofuata. Hapo huwa wachezaji wameshapata adhabu kutokana na makosa yao na pia klabu huwa imeshaadhibiwa kwani watamkosa mchezaji huyo kwa mechi mbili zitazofuata.

Je, hatua gani inachukuliwa kwa waamuzi ambao wengi wao huwa mara nyingi hawafuati sheria za uchezeshaji ama mara nyingine huonekana kama hajajifunza kabisa jinsi ya kuchezesha soka? Wengine wanazidi kutia aibu kwa kupendelea timu ambayo inampigia kelele na kumlaumu ama kumtisah kwenye kiwanja.

Utamuona mwamuzi analikubali bao na baadaye hubadilisha uamuzi huo na kulikataa. Je, ni timu gani itakayokubali uamuzi aina hiyo? Tunashangilia sana uamuzi wa KFF wa kuwapiga faini na kuwafungia baadhi ya waamuzi waliofanya makosa ambayo yangehatarisha uendeshaji mwema wa soka na hili litakuwa ni funzo kubwa kwa wapiga vipyenga ambao wanachukulia kupiga kipenga kwao kama leseni ya kuonea vilabu wasivyovipenda.

MAREFA WAADHIBIWE

Wakati umefika kwa KFF Pwani kutoa adhabu kali kwa waamuzi wanaejaribu kuharibu mechi pamoja na wale ambao hawatimizi wajibu wao kwa manufaa ya mchezo. Lazima KFF ikubaliane na mapendekezo ya kamati ya adhabu ambayo mara nyingi inapendekeza hatua kali zichukuliwe kwa marefa wanapatikana na makosa na kuonyesha wao ndio wanaosababisha kuharibika kwa mechi kadha za hapa Mombasa.

Twangoja kwa hamu kuona kama hatua zitachukuliwa na kama hatua hizo zitakuwa za mafunzo kwa waamuzi wenye nia mbaya wakiwa uwanjani.

Abdulrahman Sheriff.

VSHINDI mwingine wa Mashindano ya Maendeleo ya Wanawake uliyotayarishwa na Coca-Cola Hassan Mohammed akipokea zawadi yake ya Friji kutoka kwa Mwenyekiti wa Tawi la akina mam Bi. Mary Mwamodo huko meneja wa Coast Bottlers Mohamed Qoyyan akitazama. PICHA: NATIONAL STUDIO

HARAMBEE YA KANISA

SALAMU katika jina la Bwana wetu Jesu Kristo. Ninafuraha kwa niaba ya Parish Council kuwakaribisha katika siku hiyo Soko la Kanisa kuleta na kununua kwa mchangoi wa pesa. Tutafanyia mambo yote kwa Hall na kwa uwanja wa kanisa. Tutaanza kuuza vitu saa nne asubuhi nakuendelea. Kufungua Harambee kirasini ni saa nne mchana•

J. W. Mwadime, Provost/Mombasa Memorial Cathedral.

Namna Imam Husein alivyouawa kikatili na maadui wa Uislamu

Na Ahmed Badany Bin Muhamed Al Husseiny.

[illegible]-alipokua Kha[illegible] hamu yake ila ni kuua watu ambao walikataa kumpa voti yeye tangu wakati wa uhai wa babake. Yazid akaandika barua akampelekea Governor wake aliyoko Madina isemayo hivi:—

"Ama baadu, mshike Husain na Ibnu Umar na Ibnu Zubeir kwa voti kinguvu mpaka wakubali! Sayyidna Husein alipopata khabari ile akatoka usiku huwo hywo akaenda Maka (Mecca) Alipofika huko akapata barua nyingi sana kutoka Kofa Iraq kwa watu wa huko wanamtake aenda ili awe Khalifa kiongozi wao na waislamu wote. Sayyidna Husein akawajibu kwa a takwenda. Jawabu ya barua zao alimpa Muslim bin Akil mtoto wa ami yake, akamttuma aenda huko Iraq na akafika amletee barua amjuliza khabari za huko".

Muslim bin Akil akaenda akafika huko Kofa na watu wa huko kwanza wakamfurahikiya. Akapeleka barua kwa Sayyidna Husein ili aende haraka.

Yazid alipopata khabari ile akamuuzulu yule Governor na kule Kofa kua hakuweza kumfanya kitu yule mjumbe wa Husein. Akamuondoa yule Numan akamweka Ibnu Ziyad.

Ibnu Ziyad alikua mtu mbaya sana. Alikua dhalimu, jibari na muuwaji. Alipokwenda Kofa akawatisha watu wa huko kua, ikiwa watamshikiza yule mjumbe wa Husein, basi atawafunga na kuwaashibisha na kuwauwa. Kisha baada ya watu kutishika na wengine kupawa madonga ya pesa Ibnu Ziyad akafanya hila akamshika yule mjumbe wa Husein, Muslim bin Akil akamuuwa vibaya kabisa.

Huku Sayyidna Husein hana habari. Akatoka yeye na watoto wake, waume na wake, wakatoka Maka kulekea Iraq. Watu wengi walimkataza Sayyidna Husein asende Iraq, lakini vipi Sayyidna akakataa mwito kama huwo na ilhali ameshawapa ahdi kua atakwenda na amemtanguliza Ibnu Akil. Kadhalika vipi atakataa kuwokoa Uislamu kuutowa mikononi mwa wadhalimu.

Ibnu Ziyad alikua ameshaweka jeshi kubwa lisiopungua watu 30000 au zaidi, kupambana na hao watu wa Husein 72 tu! Jeshi hilo kubwa la maadui likenda mpaka hapo Karbala likayazunguka maji ya mto wa Furat kabla ya Sayyidna Husein hajafika.

Imam Husein maskin akifika Karbala akakuta mambo ni kama hayo, akataka kurudi Maka pia asikubaliwe, aliemkataza ni Hur kwa amri ya Ibnu Ziyad, lakini huyu Hur, mwisho atatubia atarudi kwa Husein kama utakavyosoma mbele. Akalazimishwa Sayyindna Husein apige kambi hapo Karbala Imam Husein akakaa Karbalaa siku tatu bila maji. Alikutazwa maji yeye, wanawake na watoto wa changa, Maji ya Furat yakinwea na wanyama, punda, majibwe, anakatazwa mjukuu wa Mtume (SAW).

Imam Husein aliwambia watu wake: "Hawa madui wanitaka mimi basi ubora muende zenu. Huno usiku umewafanika (kwa giza lake), basi ufanyeni ni ngamiye musafiri muende zenu. Lakini watu wake wakakataa wakamjibu: "Wallahi tutapigana pamoja nawe. Mungu ayafanya mabaya baada yako".

Hapo ilipofike siku ya tatu, nayo ni Al Juma, mwezi kumi (Ashura), mwezi wa Muharram, mwaka wa 61 Hijra. October 10, 680 A.D. Aliondoka Sayyidna Husein kupanga watu wake, kujieka tayari, mara akawaona maadui wamekuja karibu na mafarasi wao na mbele yao ni yule adui mal-uni Shimr.

Sayyidna Husein alipanda Farasi wake akapiga ukelele kwa sauti kubwa kuwaita: "Enyi watu wa Iraq! Enyi watu sikizeni maneno yangu wala musifanya haraka kuniwa, mapaka niwaidhe".

KHUTBA

Akatowa khutba ndefu Sayyidna Husein kisha akasema: "Kumbukeni mimi ni mtoto wa Binti wa Mtume wenu . . ." Maadui wakamjibu kua hawafahamu hayo anayo wambia, na wakakanusha kuwa wao walimwita!

(Itaendelea)

WAZIRI mdogo wa Kazi na Mwenyekiti wa Kanu Tawi la Mombasa Bw. Shariff Nassir akipokea mchango wa Shs 1,000 kutoka kwa mbunge wa Mombasa kaskazini Bw. Said Hemed alipoongoza Harambee ya kusaidia waliopatwa na ajali wakisafirisha maiti ukambani. PICHA: ABEID KARAMA



WAISLAMU wote wa Afrika Mashariki waomboleza kifo cha Sheikh Abdalla Saleh Al-Farsy kilichotokea Muscat, Oman Jumatatu usiku.

JISHINDIE

MIAVULI AU T-SHIRT MARIDADI KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD NO 151

KWENDA KULIA:

2. Samaki wa maji ya baridi (ziwa)
8. Ufupi wa ana mkuki
9. Tapia, kimbilia
10. Tapanya, weka mbalimbali
11. Mti wa mahindi au mtama
13. Baa
14. Asali
17. Pamoja na
18. Jina la Kijaluo
21. Nikahi arusi
22. Unywele uliyo juu ya jicho
23. Aitoe maganda

KWENDA CHINI:

1. Uzi mnene
2. Ghairi
3. Afunga ndoa
4. Jina la Kiume
5. Kinyume cha hana
6. Uliyoruzukiwa, chakula
7. Jina la zamani la shirika la ndege Afrika Mashariki
12. Ujuzi uhodari
14. Upeleke ujumbe wa kuoa
15. Ikimbilie, itapie
16. Neno la kuitikia
18. Angalia, tizama
19. Wingi wa yake ukizipanga herufi sawa
20. Sehemu ya kiwiliwili.



Washindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 150

1. Kibwana Juma Mzee Sanduku la Posta 85404 Msa.
2. Athman Abdallah Ali Sanduku La Posta 29 Kilifi.
3. H. J. Chika Sanduku La Posta 90520 Mombasa.

Washindo waombwa wafike afisini mwa *COASTWEEK*.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 150 —

KWENDA KULIA:

1. MAGUGU, 5. PUMU, 7. SONARA, 8. BT, 9. A.A., 10. MBOGO, 12. ANGIKA, 14. TU, 15. AU, 16. UMUKA, 18. UMO, 19. LAU.

KWENDA CHINI:

1. MASHUA, 2. UTAMBI, 3. UPANGA, 4. OMBA, 6. UTAMU, 10. MGUU, 11. OKOA, 13. NAMI, 14. TIMU, 17. KU.

JINA ....

SANDUKU LA POSTA ....

....

Shindaano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata miavuli au T-Shirt maridadi. Shindano hili limeshaminiwa na *COASTWEEK* Limited Mombasa.
Jawabu za Fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri *COASTWEEK* Sanduku La Posta 87270 Mombasa, Kenya.
Siku ya Jumatano tarehe November 24, 1982 saa nne asubuhi shindano hili litakuwa mwisho.